MAJIBU YENYE FAIDA NO.3

KUHUSU

MASWALI YANAYOFUNGAMANA NA MIFUMO MIPYA

MTUNZI: SHEIKH SWALEH BIN FAWZAN BIN ABDILLAH AL FAWZAN

MFASIRI: ABUL AALIYAH UMAR BIN MUHAMMAD BIN KONDO

PONGWE - TANGA – TANZANIA

SWALI LA TATU:

Nataraji kuwekewa wazi: Ni yapi makusudio ya (msamiati huu)"Fiqhi al waaqi´i" kwa sababu hali ilivyo hakika limeachiwa (limeitwa) tamko hili na limekusudiwa kwalo tamko la kilugha,na si tamko la kisheria?

JIBU: Wanasema: Katika ugumu ni kukiweka wazi kilichokuwa wazi.

Fiqhi inayotakiwa na Fiqhi inayopendezeshwa nayo ni Fiqhi ya kitabu na sunna, hii ndio Fiqhi inayotakiwa,ama Fiqhi ya Lugha hiyo ni katika vilivyoruhusiwa ni jambo lilinalotakiwa kwa watu,unajifundisha katika lugha,unaelewa maana ya neno na mipasuko yake na herufi zake na kadha na kadha… na hii inaitwa Fiqhi ya lugha kwa mfano: kitabu "Fiqhu al Lugha" cha al-Tha´alabiy na

wengineo,haya ni katika mambo yanayokamilisha na ni katika kujifundisha Lugha.

Ama (tamko)"Alfiqhu"litakapoitwa kama lilivyokuja katika kauli yake ta´laa: "..***wakajifunze vyema Dini..***"[1].

Na kauli yake Mtume swallallahu ´alayhi wsallama:

" ***Yule ambaye Allah akimtakia kheri humfahamisha katika Dini***"[2].Na kauli yake ta´laa :

(*Basi wana nini watu hawa hata hawakaribii kufahamu maneno..)?*[3].

(***Lakini wanaafiki hawafahamu***…)[4] na nyinginezo katika aya na hadithi.

Muradi wa hayo ni kuwa na uelewa katika Dini kwa kuzijua hukumu za kisheria hili ndilo

---

[1]- Suratu al-Tawbah aya ya (122).
[2] - Al Bukhariy (71) Muslim (1037)
[3] - Suratu al-n-Nisaa aya ya (78)
[4] - Suratu al Munafiquna aya ya (7)

linalotakiwa,na hili ndilo ambalo inawapasa waislamu kulitilia umuhimu na kujifunza hilo.Lakini si makusudio ya Fiqh al waqi´i kwa hawa, Fiqhu al lugha,bali makusudio kwa tamko hilo kwao ,ni kujishughulisha na mambo ya kisiasa na hamasa (uchochezi) za kisiasa na kutumia wakati na hima kwenye jambo hilo.

Ama Fiqh al ahkaami (kuelewa hukumu za kisheria) wanaziita Fiqhu al juz´iyyaati na wanaziita Fiqhu al haydh na an-n-Nifasi (Fiqhi ya hedhi na nifasi kuelewa mambo ya hedhi na nifasi tu) ili kudharau Fiqhi hiyo na kuwaepusha -watu- na fiqhi hiyo na wasishughulike nayo.